# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 1 – NGUVU YA AGANO

**LENGO:** Kuwapa wanandoa uelewa wa ndani wa maana na nguvu ya agano, baraka zinazoendana na mahusiano ya agano pamoja na Mungu, na faida za agano la ndoa kwa wale walio ndani ya Kristo.

**MAELEKEZO:** Wape fursa wale wanaotaka kumpokea Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wao. Hii inaweza kufanyika baada ya somo, wakati wa mkazo maishani, au wakati wa mjadala kwa wiki ijayo.

**KULENGA KUOMBEA:** Ombea dua washirika wote waliomo kwenye kikundi ambao bado hawajaokoka. Ombea wanandoa kuweza kuelewa undani wa mahusiano ya agano. Ombea maarifa kuhusiana na mahitaji ya wanandoa wako. Anza kuombea sasa kuhusu matoleo ya kila wiki, kwa ajili ya wanandoa kuelewa jinsi wanavyobarikiwa.

## ✦ DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

### NINI CHA KUFANYA

Wakaribishe wanandoa nyumbani kwako. Ruhusu kila mmoja awashirikishe wenzake habari zake binafsi – wameoana kwa muda gani, watoto wangapi, n.k. michezo ya burudani inaweza kuwa msaada mkubwa sana kuwafanya wanandoa wajisikie huru. Unaweka mazingira sahihi kwa ajili ya hapo baadaye kadiri mnavyoendelea kuwa pamoja. Saidia kuweka mazingira sahihi, mazingira ya kirafiki.

Waeleze kuhusu tovuti yetu www.2equal1.com

### VYETI

Waache wanandoa **WAANDIKE** majina yao, anwani, na namba za simu kwenye Taarifa ya Mguso kwa wiki ya kwanza (ona sehemu ya fomu mwishoni mwa matini hii). ***Jinsi majina yanavyoonekana yameandikwa kwenye fomu hii ndivyo yatakavyoonekana kwenye vyeti vya kuhitimu*** hivyo hakikisha kuwa ni rahisi kusomeka na ni majina wanayotaka yatumike kwenye vyeti vyao.

### MAOMBI YA UKARIBISHO

Fungua kwa maombi mafupi kwa kumshukuru Bwana kwa ajili ya kile ambacho atakitenda kwa kila ndoa ya wanandoa.

### MAELEKEZO YA DARASANI

Pitia maono, muundo wa shirika, na hali ya kujitoa kwa dhati iliyoko kwenye ukrasa wa 7 na 9 na kile unachotarajia kwenye ukrasa wa 8. Zungumzia kuhusu Kumshirikisha mchungaji (ukrasa wa 9). Waombe wanandoa wasome na kutia sahihi kwenye sehemu ya kujitoa kwa dhati iliyoko ukrasa wa 9.
Maadili na misingi ya shirika imetajwa ukrasa wa 8 wa matini ya wanandoa. Wanandoa wanaweza kusoma kwa muda wao, lakini acha wajue kwamba uko wazi kuzungumzia cho chote wanachouliza au hawajaelewa.

### KUTOA FURSA

Wiki hii ya kwanza ni vizuri kushirikishana namna darasa litakavyoendeshwa. Pia ni muda mzuri kueleza kwa nini watakuwa na fursa ya kutoa kifedha na namna ambavyo fedha hizo zitakavyotumika, kwa nini hakuna maswali wakati wa kufundisha, ni maswali gani yanahitaji ufafanuzi, n.k. Pia ni wakati wa kuweka mazingira sahihi kwa wanandoa wanaoondoka mara kipindi kinapokwisha ili Roho Mtakatifu aanze kutenda kazi ndani yao kila mtu binafsi.

### FUNDISHA SOMO

Fuata mwongozo wa ukarasa wa 29 kwa kufundisha na uhitimishaji wa kipindi.

### Mahojiano ya Pili

Tumekupa sehemu moja ya mahojiano kwa kila somo. Waelekezaji wa Ndoa wengi wameomba mahojiano **ya pili** kila wiki.

Kama utapenda kufanya mahojiano ya **pili**, unaweza kuchagua mada na swali. Hakikisha mahojiano hayo yanachukua dakika tatu.

Pamoja na mahojiano uliyopewa, hii inakupa fursa ya kutoa mahojiano kwa mara ya pili na utayari wa kubadili mada kila wakati unapofundisha kama utapenda.

* Usisahau kwamba maneno yaliyopigiwa mstari lazima yatumike katika kufundisha.
Haya ni maneno ambayo wanandoa watakuwa wakiyatafuta ili kukamilisha maelezo yao ya kitabuni.

↳ Ona sehemu ya fomu ambayo iko nyuma mwa matini hii kwa ajili ya kukusaidia kukamilisha Fomu za Mguso kwa kila wiki.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 2 – NGUVU YA 2=1

**LENGO:** Kupata uelewa wa nini hutokea pale 2 inapokuwa sawa na 1 na iliumbwa kuwa nini, na jinsi gani mpango wa Mungu ulivyoingiliwa na anguko la mwanadamu, na kwamba Yesu amewakomboa wanandoa na kuwarejesha katika mpango wa asili wa ndoa.

**MAELEKEZO:** Kumbuka somo hili linalenga nguvu ya ndoa kama Mungu alivyoiumba, siyo kuachana na kuoa au kuolewa tena. Huo ni mtazamo mmojawapo wa somo hili. Usiruhusu liwe lengo lako. Wasaidie wanandoa kuona uwezekano wa mahusiano yao ya pamoja na nguvu ya Mungu ikitenda kazi kwa niaba yao. Wakati wa mjadala ruhusu kila mwanandoa kushirikisha uzoefu wake wa wokovu na imemaanisha nini kwake. Baada ya kipindi wahudumie wanandoa wanaohitaji msaada.

**KULENGA KUOMBEA:** Endeleza dua kwa ye yote ndani ya kikundi ambaye hajampa Yesu maisha yake. Wakumbuke katika maombi wanandoa wale waliotubu na kufunguliwa katika jina la Yesu kutoka katika hukumu. Omba kadiri Roho Mtakatifu anavyokuongoza. Omba kwa ajili ya uaminifu katika utoaji.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

MIONGOZO YA KILA WIKI KWA AJILI YA NDOA NI YA KUDUMU KWA WIKI YA 2-12

- **Muda wa ushirika. Dakika 10-15**

  Watie moyo wanandoa kufika dakika 10 hadi 15 kabla ya kipindi kuanza ili kwamba waweze kusalimiana na kujuliana hali. Wanandoa kufika, wanapata chai au kahawa, n.k., na kujuliana hali kila mmoja na mwenzake.

  Huu ni muda maalum sana kwa wanandoa, hivyo watoto hawaruhusiwi katika vipindi vya Ndoa ni ya Kudumu.

- **KIPINDI HUANZA mara moja kwa muda uliopangwa.**

  Usiwasubiri waliochelewa kufika. Kama mwanandoa atafika kwa kuchelewa, wajiunge na kikundi kimya kimya bila kuleta usumbufu wo wote.

- **Sifa na Ibada. Dakika 10-15 (Utoaji wa fedha unaweza kufanyika wakati huu kama unataka iwe sehemu ya sifa na ibada.)**

  Uwe makini na mazingira ya wanandoa wako na weka muziki ambao Roho Mtakatifu atakuongoza kuwa ni sawa. Huu siyo muda wa kuzama sana katika sifa na ibada.

- **Kushirikishana somo la wiki iliyopita na Mkazo Maishani. Dakika 30-45**

  Kuda wa kila mmoja kutoa maelezo yake utegemee na jinsi mtu anavyokuwa wazi. Shirikisha kile ambacho Bwana amekuwa akikifanya katika maisha yako kwa wiki iliyopita. Shirikisha magumu na yale uliyoonesha ushindi kwayo.

  Huu ni muda wa mahojiano ndani ya kikundi. Kuna maswali yanayopendekezwa nyuma ya matini yako.

  Watie moyo wanandoa kuzungumza kama kikundi. Hasa jitahidi kuwashirikisha wale ambao wanaweza kuwa si wasemaji sana kama walivyo wengine.

- **Fursa utoaji wa fedha. Dakika 2-5 (Labda uwe umeifanya moja kwa moja wakati wa sifa na ibada.)**

  Ada ya kujiunga inapaswa kuwa ni kiasi kidogo ili kutoa fursa ya wengi kutoa kwa uhuru. Waambie ni muhimu kuombea kile watakachotoa kwa kila wiki.

  Mwombe mwanandoa mmoja kuombea matoleo hayo. Kisha PITISHA kapu kwa kila mwanandoa.

- **Mapumziko mafupi na/au muda wa kujisaidia. Dakika 5-10**

  Amua ni jinsi gani mtashughulikia viburudisha darasani kwenu. Baadhi ya Waelekezaji wa ndoa, hutoa viburudisho kama sehemu yao ya ukarimu. Wengine huwaomba wanakikundi kuleta cho chote watakachoshirikisha kikundi. Watie moyo wanandoa kuchukua viburudisho vyao, kutumia choo, kuwasiliana na walezi wao wa watoto, n.k. Rejesha darasa katika hali yake ya kawaida baada ya muda wa mapumziko kumalizika na anza mafundisho.

- **Mafundisho huwasilishwa kwa dakika 45-60**
- **Muda wa kuhitimisha ni dakika 1-2 (Maswali ya ufahamu, Neno ambalo halikueleweka, n.k.)**
- **MWISHO WA KIPINDI.** Baada ya kipindi, pata muda na wale walioomba hivyo au wanaohitaji msaada zaidi

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 3 – NGUVU YA USHIRIKIANO

**LENGO:** Kwa kila mwanandoa kuelewa wito WAKE maalum kutoka kwa Mungu, ukiwa umejengwa katika kielelezo cha uwajibikaji wa kibiblia wa Kristo na kanisa lake.

**MAELEKEZO: Hili siyo somo kuhusu nani kichwa na kutii! Tafadhali usifundishe kwa njia hiyo!** Kila mume na kila mke atazame wajibu wake na kutamani kufaulu katika wajibu huo. Siyo wakati wa kupinga kuchambua uwezo wa mwenzi wako. Kama mume na mke watafaulu katika jukumu lao wenyewe, ukamilifu wa mwili mmoja utajidhihirisha.

**KULENGA KUOMBEA:** Hii ni wiki ambayo ugomvi unaweza kutokea katikati ya wanandoa wako. Pigana vita vya kiroho kwa niaba yao. Mwombe Mungu akupe hekima na mafunuo kuhusiana na roho dhahiri zinazotenda kazi. Fuata maelekezo unayopewa na Roho Mtakatifu. Waombee wanandoa ili waenende kwa pamoja katika kupanda fedha kwa ajili ya huduma.

# ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

## Kufundisha Somo

Liishi somo wiki moja kabla hujalifundisha. Tumieni muda kuomba pamoja kama wanandoa kadiri unavyojiandaa kufundisha. Kila somo linawasilishwa kwa njia ya muhtasari na maelezo. Maelezo haya yanakupa wazo la jinsi gani unaweza kuwasilisha muhtasari. Tafadhali usisome maelezo wakati ukifundisha somo! Fuata mpangilio wa muhtasari kwa faida ya wale wanaoandika notisi au maelezo.

Lifanye somo liwe hai. Fundisheni kama timu ya mwili mmoja – wote mume na mke kwa pamoja. Katika nyumba yenye nguvu, wanandoa **wote** wanapaswa kuwa imara katika Roho. Mruhusu Mungu kuvunja mila na desturi, mambo yaliyotengenezwa na wanadamu ili kumfuata yeye kwa uhuru. Kumbuka kutumia kanuni kwa ***mifano binafsi*** maishani mwako. Masomo yasifundishwe na mwanandoa mmoja tu au mwanandoa mmoja kutoka kwenye kila timu ya uelekezaji.

**Hakikisha maneno yaliyokorezwa wino na kupigiwa mstari yanatumika katika mafundisho. Haya ndiyo maneno ambayo wanandoa watakuwa wakiyatafuta ili kukamilisha notisi zao.**

Wakati wa kufundisha siyo wakati wa kuhojiana. Kama wanandoa wana maswali waombe waandike maswali hayo kwa ajili ya muda wa muhtasari mwishoni mwa kipindi.

Wanandoa walio katika mafunzo wanapaswa kufundisha angalau mara mbili wakati wa kozi. Omba kwamba hayo yatakuwa ni masomo gani. Tunashauri kwamba Wanandoa waelekezaji wafundishe Somo la 1 na 2 kwa sababu ni ya msingi kwa kozi nzima. Kama wanandoa waliomo kwenye mafunzo hawajawahi kuwa kwenye kikundi cho chote hapa awali na hawajawahi kulikia somo hili, wanandoa waelekezaji lazima walipitie tena somo kabla hawajaanza kufundisha.

Dakika 1-2 za muda wa kufungasha mwishoni mwa mafunzo. (MASWALI YA UFAFANUZI)

Huu ni muda wa kufafanua—neno lililokosekana au marejeo ya Biblia ambayo hayakueleweka. Huu siyo muda wa mafundisho ya Kidoktrini au kutokukubalian. Wasihi wanandoa kwamba kama bado wana tatizo wafanye kwanza mkazo maishani na kuona kama baadhi ya maombi yao hatajibiwa.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

**WIKI YA 4 – NGUVU YA KUPANDA NA KUVUNA**

LENGO: Kuwa makini na mchakato endelevu wa kupanga na kuvuna katika ndoa. Kujua jinsi ya kuchagua mbegu na jinsi gani ya kufanya kuhusu mazao hafifu.

MAELEKEZO: Watie moyo wanandoa wako kutunza mawazoni mambo yale mazuri waliyokwisha kupanda. Kuna tabia ambayo hujitokeza katika somo hili, tabia ya kukata tamaa na kutazama mazao hafifu peke yake. Watahadharishe dhidi ya mtego huu.

KULENGA KUOMBEA: Omba dhidi ya roho ya kukata tamaa na ugomvi. Mtafuta Roho Mtakatifu maalum kuhusu wanandoa wako. Waombee wawe na moyo laini ili kupokea mafundisho yafuatayo kuhusu msamaha. Waombee wanandoa ili kuielewa kanuni ya kupanda fedha na kuvuna wakipenda fedha wiki hii.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

## Huduma Baada ya Darasa

Wale wanandoa ambao wanahitaji msaada zaidi watiwe moyo ili waweze kubaki baada ya kipindi ili wapewe huduma. Usitumie muda wa kipindi kwa ajili hiyo. Huduma kwa wanandoa lazima iwe ni ya mwili mmoja, wanandoa kwa wanandoa. Ruhusu Roho Mtakatifu akuongoze ni kwa namna gani na lini uweze kuhudumia. Anajua hitaji la kila mwanandoa na atatoa muda wa namna hiyo. Usiwe na wasiwasi kwamba itakuwaje.

Kwa kawaida ni wanandoa viongozi tu ndiyo wanaoruhusiwa kuhudumia. Wengine waruhusiwe kuondoka ili kumruhusu Bwana aendelee kufanya kazi katika ndoa zao wenyewe. Mwe wazi, hata hivyo kwa maelekezo ya Roho Mtakatifu kuhusiana na wanandoa wengine wanaotumika pamoja nanyi.

Kumbuka, lengo letu ni kuwasaidia wanandoa waweze kujifunza kusikia wao wenyewe kutoka kwa Bwana. Tunataka kuwaongoza na kuwapitisha katika maeneo ambayo “wamekwama” lakini hatutaki kuwa sauti ya Mungu kwa ajaili yao. Mara zote, watie moyo wanandoa kuutafuta uso wa Bwana kwa ajili yao wenyewe huku wakipata msaada kutoka kwenu. Ni ndoa yao hivyo wanapaswa kuwekeza wao wenyewe.

## Mahudhurio

Baada ya kuanzisha kikundi, wanandoa wanapaswa kuhudhuria kila wiki. Kama mwanandoa mmoja hawezi kuhudhuria kikao, basi yule mwingine ahudhurie na kumshirikisha mwenzake somo hilo. Kama wote wawili hawakuhudhuria, **ni uamuzi wa Wanandoa Waelekezaji kuwapatia somo hilo au la**. Baadhi ya wanandoa hupendelea kuhudumiwa mtu mmoja mmoja na watatumia fursa hiyo kukutana nawe binafsi. Wanandoa wengine watakuwa na hamu ya kulipata somo hilo walilolikosa. Wasiliana nao. Mwombe Bwana akuongoze nini cha kufanya pale mwanandoa asipohudhuria kwa muda wa wiki nzima.

**Kusiwe na kumbukumbu ya mahudhurio. Somo moja tu ndilo lifundishwe kila mkutanikapo. Usichanganye masomo.**

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 5 – NGUVU YA MSAMAHA

**LENGO:** Kuelewa maana halisi ya msamaha, kutambua umuhimu wa kusamehe, na kujifunza JINSI ya kusamehe.

**MAELEKEZO:** Jitayarishe kukabiliana na wale walioshikilia chuki au hali ya kutokusamehe mioyoni mwao na hawataki kuachilia. Baada ya kikao toa huduma maalum kwa wale wanaohitaji msaada maalum katika kukabiliana na mkazi maishani wa wiki hii.

**KULENGA KUOMBEA:** Msamaha ni ufunguo katika uponyaji na uimarishaji wa ndoa. Pia ni ufunguo kwa afya ya kimwili na kiakili. Waombee wanandoa ili wasione tu kwamba msamaha ni wazo zuri, bali umeamriwa na Mungu. Kuwaona watu kama Mungu awaonavyo hakutusaidii tu kuwasamehe bali na kuachilia neema na baraka kwao pia.

Endelea kuwaombea wanandoa wako kadiri wanavyomruhusu Bwana kusafisha mioyo yao. Endeleza vita vya kiroho kadiri Roho Mtakatifu anavyokuongoza ukisisitiza watu wasilipize kisasi na kutunza uchungu ndani ya mioyo yao.

Hapa ndipo mahali pa kufanyia mageuzi yenye nguvu na mioyo ya wanandoa ibaki laini ili kupokea kile Bwana alichowatunzia. Omba kwamba kama wanandoa wameshikilia uchungu dhidi ya makanisa au huduma kuhusiana na mambo ya fedha, watasamehe ili kuruhusu kuongozwa na Roho wa Mungu. Kaa macho kwa maelekezo yake wakati wa maombezi ya wanandoa. Ombea mapema kuhusu wanandoa wanaohitaji kubatizwa na Roho Mtakatifu.

# ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

## Kwa nini idadi ya juu ni wanandoa saba tu?

### Kwa nini tunapendekeza kuwa na wanandoa saba tu katika kila darasa?

Ndiyo, kwanza kabis ani kwa sababu ndiyo maelekezo ya Bwana aliyoyatoa wakati alipotoa mwongozo wa kozi hii. Hapo mwanzo, tulikuwa tunatii sana maelekezo yake, lakini tuliweza kuongeza wanandoa hapa na pale kutokana na mwingiliano wa ratiba. Lakini tuligundua kwamba elimumwendo au uhai wa darasa ulibadilika kila mara tendo hilo lilipofanyika.

Tangu hapo tulifanya kazi yetu ya nyumbani na kujifunza kwamba hali ya ukaribu wa ndani katika kikundi (hali ya kujisikia vizuri na kushirikishana mambo kwa uwazi zaidi) hubadilika sana pale kunapokuwa na zaidi ya wanandoa kumi na nne. Watu kumi na nne watashirikishana kwa undani sana kuliko kumi na tano au zaidi.

Cha kushangaza. Roho Mtakatifu alitupatia maelekezo ya wazi kabisa!

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 6 – NGUVU YA IMANI

**LENGO:** Kuwasaidia wanandoa kuyatambua maono ya imani kuwa ni nini, jinsi ya kuandaa, na umuhimu wa kuwa nayo kati ya mtu na mwenzake na kwa mahusiano ya mwili mmoja.

**MAELEKEZO:** Waonye wanandoa dhidi ya tabia ya kuorodhesha makosa ya wenzi wao na kuyafanya kuwa orodha ya kuangalia jinsi Mungu anavyoshughulikia moja baada ya lingine. Hili ni ono la Mungu la kiimani kwa kila mmoja.

**KULENGA KUOMBEA:** Unakwenda kuona kazi ya ndani kabisa inayofanyika ndani ya kila mwanandoa kwa Roho wa Mungu. Endelea kuwa makini wakati wa maombezi yako kwa wanandoa. Waombee mapema wanandoa ili waweze kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ombea wanandoa wako wapewe imani mpya kuhusiana na pesa zao kadiri wanavyojiandaa kutoa fedha zao kwa wiki hii.

# ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

## Matoleo Yanakwenda Wapi?

Hili ni swali halali kabisa. Watu wangependa kujua pesa inayotolewa inakwenda wapi.

Gharama za uendeshaji zimebakizwa chini sana. Huko Marekani, hakuna kiongozi anayepokea mshahara, wakiwemo waanzilishi wa maono haya. Wafanyakazi wa ofisini ni wachache tu. Wakti tukiandika haya ni watumishi watatu tu ndio wanaopokea mshahara, na wawili hufanyakazi kwa masaa.

Huduma inamiliki jengo ambamo ofisi zake zimo na kodi ya majengo katika vyumba vingine vya majengo hutoshereza gharama za huduma hii. Lengo letu ni kutumia kiasi kidogo cha fedha kadiri inavyowezekana kwa mambo ya utawala ili kwamba fedha inayobaki iweze kwenda kutumika kuwafikia wanandoa wengi ulimwenguni kote.

Gharama ya usajiri wa darasa hutumika kugharimia vifaa na usafirishaji. Matoleo ya wanandoa hutumika kama matoleo yanayosaidia huduma hii kuwafikia wanandoa wengine huko Marekani na ulimwenguni kote. Fedha hizi husaidia kufundisha viongozi wapya, kutafsiri vitabu na maandiko mbalimbali katika lugha ambazo tunawafikia watu wa nchi hizo.

Gharama kwa ajili ya kozi imeachwa chini sana kwa sababu tunataka wanandoa wautatute uso wa Bwana ili awaongoze jinsi ya kutoa. Tunajua kwamba wanapotoa wanabarikiwa, hivyo tungependa kuona wanabarikiwa badala ya kujisikia kwamba wanalipia kozi tu.

## MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI,
### WIKI YA 7 – NGUVU YA UKARIBU WA KIROHO

LENGO: Kwa wanandoa kutambua umuhimu kwa nini lazima waombe pamoja, jinsi ya kuomba pamoja, na umuhimu wa ubatizo wa Roho Mtakatifu.
MAELEKEZO: Uwe tayari, kufuatilia kikao, kumwongoza ye yote anayetaka Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Uwe makini na jinis ambavyo Roho Mtakatifu atakavyomhudumia kila mtu, kuna wakati atafanya hadharani na wakati mwingine kibinafsi. Atakuongoza. Kuna upako maalumu katika 2=1 ili kuwasaidia watu kupokea lugha yao ya maombi pale wanapobatizwa. Tunaaamini hii hutokana na umuhimu wa wanandoa kuomba kwa pamoja, hasa katika Roho. Tembea katika nguvu ya upako huu kadiri unavyohudumu.
KULENGA KUOMBEA: Endelea kuombea ye yote yule anayetaka kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Anza kumtafuta Bwana kwa ajili ya viongozi wanaotarajiwa kupatikana kwa ajili ya Mafunzo ya wanandoa kwa kila kikundi. Endelea kuomba maalumu kadiri Roho anavyokuongoza. Endelea kuomba kwamba kadiri wanandoa wako wanapoendelea kuomba kwa pamoja, watamwuliza Mungu kuhusu sehemu yao ya kifedha watakayotoa kwa ajili ya huduma hii.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

### Neno Kuhusu Kuomba katika Roho kutoka kwa Mike na Marilyn Phillipps

Miaka mingi iliyopita tulipanga mpango wa kukodi mabasi mawili kwa ajili ya usafiri wakati wa mkutano mkuu wa mwaka. Mara tuligundua kwamba kuendesha basi ilihitajika kuwa na leseni maalumu linalokuruhusu kuendesha gari la abiria. Tulijaribu kuwaeleza maafisa kuhusu uzoefu na kumbukumbu nzuri za madereva wetu, lakini maafisa hao hawakuonesha dalili za kuelewa tulichokuwa tukiwaeleza. Wao walisisitiza kwamba kama wanataka kusafirisha watu kwa kuendesha magari ya abiria lazima wawe na leseni inayowaruhusu kufanya hivyo. Walieleza kwamba kuendesha gari lenye abiria kulihitajika vigezo tofauti kabisa ukilinganisha na vile vya kuendesha gari lako binafsi. Kwa hiyo, kutokana na ukweli kwamba hakuna hata mmoja wetu aliyekuwa na leseni ya jinsi hiyo, ilitulazimu kukodi madereva waliokuwa na vigezo hivyo.

Wale maafisa walipokuwa wakisisitiza kwamba wale madereva wetu lazima wawe na leseni halali ya kuendesha magari ya kubeba abiri, je, walikuwa wakituambia kwamba madereva wetu walikuwa ni raia wa daraja la pili? Je, walikuwa wakisema kwamba madereva wetu walikuwa na kumbukumbu mbaya za udereva? Je, walikuwa wakisema kwamba watu wenye leseni halali ya kuendesha magari ya kubeba abiria walikuwa bora kuliko wale wasiokuwa na leseni hizo? La hasha! Walichokuwa wakikisema ni kwamba kuendesha basi la abiria kulitakuwa mafunzo na stadi tofauti na zile za kuendesha gari la binafsi.

Hivyo watu wanapotafuta nafasi za kazi hugundua kwamba kazi mbalimbali zinahitaji vigezo tofauti tofauti. Baadhi yake huhitaji shahada ilihali zingine huhitaji uzoefu wa aina fulani. Je, uzoefu huo humaanisha kwamba wale wasiokuwa nao ni dhaifu au hawafai kwa wale walionazo? Je, inaweza kukubalika kuamini kwamba waajiri walio na vigezo fulani si wazuri au ni wakatili? La hasha! Vigezo wanavyoorodhesha, kama tu ilivyo leseni halali ya kuendeshea gari la kubeba abiria, hutegemea mahitaji ya kazi yenyewe. Bila kukidhi vigezo, itakuwa vigumu sana kukidhi mahitaji ya kazi yenyewe.

**Ndivyo ilivyo katika uongozi wa *2=1*. Katika masomo yote ya Kuelekeza Wanandoa kuna nyakati nyingi ambazo wanandoa wanatiwa moyo kuomba katika Roho. Wiki ya Nne inatanguliza wazo la kuomba katika roho. Wiki ya Saba hufundisha wanandoa umuhimu wa kuomba kwa pamoja, iwe katika lugha zao za asili na katika roho. Somo hili linatanguliza Ubatizo wa Roho Mtakatifu na kuwaambia wanandoa kwamba wanandoa waelekezaji wao wataomba pamoja nao kama watapenda kupokea ubatizo wa roho na karama, ikiwemo kunena kwa lugha. Wiki ya Nane huwafundisha wanandoa jinsi ya kukubaliana kwa njia ya maombi ya pamoja katika roho mpaka wanasikia kitu kile kile kutoka kwa Bwana.**

Kila moja ya masomo haya yanamtaka kiongozi kufanya kitu alichonacho uzoefu, siyo tu kile walichokisikia. Haitoshi tu kuwa na ufahamu wa kinadharia. Watu wanaoendesha magari binafsi, bila shaka wanayo nadharia ya jinsi ya kuendesha basi la kubeba abiria. Hiyo haikutosha kwa abiria basi la abiria.

Tunapodai kwamba viongozi wa ***2=1*** lazima wabatizwe katika Roho Mtakatifu na kuwa wazi kwa karama zote, hatusemi kwamba wao ni wazuri zaidi yaw engine au kwamba wana karama zilizo nzuri zaidi au wao ni Wakristo wazuri zaidi. Kuna watu wengi ambao hawajabatizwa katika Roho Mtakatifu ambao wana ndoa nzuri tu kuliko wale waliobatizwa. Pia wanaweza kuwa washiriki wazuri wa kanisa au kuwa na tabia na uwezo mzuri zaidi.

Kubatizwa katika Roho Mtakatifu na kuwa wazi kwa karama zote ni vigezo muhimu kwa wote wanaotaka kuwa waelekezaji wa wanandoa wa ***2=1*** kwa sababu wanahitaji hayo ili kufundisha madarasa yao. Sisi sote wawili tulipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu bila udhihirisho wa kunena kwa lubha. Wote tulipata uzoefu wa kuzuwiwa vitu mbalimbali vilivyotutenganisha ili tusipokee kile Maandiko yanasema. Tulikuwa tumezungukwa na watu, ambao ingawa walilijua neno la Mungu walitutia moyo kuitafuta kweli ya Neno.

Ni muhimu kwa waelekezaji wa ***2=1*** kuwa na utayari wa kuendelea na wanandoa, wakiwasaidia katika mambo yanayowazuia Mungu asitembee katika maisha yao. Hii inawezekana tu pale Ubatizo wa Roho Mtakatifu na karama ya kunena kwa lugha vinapokuwa siyo jambo la nadharia tu bali sehemu muhimu ya maisha ya mwelekezaji.

Tunasisitiza sana Ubatizo wa Roho Mtakatifu katika maisha ya kila mmoja aliye sehemu ya mwili wa Kristo. Ni zana muhimu katika hazina yetu ya silaha, chombo cha sifa, na “simu yetu ya kazini” kwa kamanda wetu mkuu, Yesu, katika joto la vita vya kiroho. Tunaamini kwamba kila muumini lazima awe nayo karama hii kama faida na baraka binafsi. Zaidi sana tunaisisitiza kwa waelekezaji wa ***2=1***. Kwao ni vigezo muhimu vya kazi.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

## WIKI YA 8 – NGUVU YA MAPATANO

**LENGO**: Kutambua sababu za kukubaliana, kujifunza namna ya kukubaliana kwa njia ya Mungu, na kujifunza jinsi ya kufikia makubaliano kwa njia ya Mungu.

**MAELEKEZO:** Wakati wa majadiliano fuatilia wale ambao wameweza kubatizwa katika Roho Mtakatifu kwa wiki iliyopita. Jiandae katika Roho kuwa tayari kukabiliana na mabishano ya kidoktrini kulingana na maelekezo yaliyoko mwishoni mwa somo la 7. Ukifuatilia kikao, saidia kuwaweka huru wale wanaotaka lugha huru wakati wa maombi.

**KULENGA KUOMBEA:** Endelea kuwaombea wanandoa. Roho Mtakatifu anashughulikia maeneo fulani ambayo hapo kwanza hakuwa na kibali cha kuyafikia. Usikate tamaa—endelea kwa ajili ya wanandoa wako. Omba kwamba watafikia makubaliano kuhusu utoaji wa fedha zao kwa kila wiki.

# ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦

## WAJIBU WA WAELEKEZAJI WA NDOA NI YA KUDUMU

### Kwa Wanandoa wa Darasani Kwako

- Omba pamoja na waelekezaji wako wa Mafunzo kwa ajili ya wanandoa wote waliomo darasani, mkipigana vita vya kiroho kwa niaba yao na kukubaliana na maono ya Bwana kwa ajili ya kila mmoja wao.
- Watie moyo wanandoa wa darasani kwako na kuwaelekeza kukabiliana na maeneo magumu maishani mwao.
- Kumbuka, hufundishi tu, bali uwe kielelezo pia. Ni mchakato, siyo ukamilifu.
- Hakikisha kwamba kila mwanandoa darasani kwako anatambua umuhimu wa kushiriki kila wiki.
- Mpe maono kila mwanandoa kwamba Mungu ana mpango kwa ajili ya ndoa yao na uwasaidie kuufahamu mpango huo.
- Jibu maswali yao kwa uaminifu na tafuta msaada wa majibu kwa maswali usiyojua majibu yake.
- Tulia na uwe halisi.

### Kwa Waelekezaji Walio katika Mafunzo

- Watie moyo waelekezaji walio katika mafunzo katika ndoa zao wenyewe na katika majukumu yao ya kuelekeza wengine.
- Fundisha masomo yote ya Ndoa ni ya Kudumu kwa darasa zima isipokuwa wale uliowateua kuwa sehemu ya mafunzo. Pitia masomo ulioyateua kwa pamoja na Waelekezaji walio katika mafunzo kabla hawajafundisha, kama hawajayasikia hapa awali.
- Hakikisha wamekamilisha hatua zote za maandalizi ya uelekezaji – video tatu (Maadili, Kuitunza Nyumba Yako, na Kuelewa Mamlaka), Kujisomea Biblia somo la Yoshua, na wamesoma kitabu cha uelekezaji cha ***2=1***.
- Omba pamoja nao kwa ajili ya wanandoa wawili ambao utahitaji waanzishe madarasa mawili mapya.
- Hudhuria mikutano ya uhamasishaji ya ***2=1***.

Kumbuka, nyumba yako ndiyo kituo cha kuwafikia majirani zako, marafiki zako na famila zao, na jumuia yako. Kadiri utakavyomruhusu Mungu kutiririka kupitia kwako, ndivyo utakavyoona miujiza mingi nyumbani mwako.

## WAJIBU WA WAELEKEZAJI WA NDOA NI YA KUDUMU KATIKA MAFUNZO

### Kwa Wanandoa wa Darasani Kwako

- Kwenye kipindi hiki mko kwenye mafunzo, hivyo jifunze kadiri uwezavyo katika majuma haya ya kozi hii.
- Wasaidie wanandoa wako wanaofanya kazi ya kuelekeza kwa njia ya maombi na wakati wa kipindi.
- Fundisha angalau masomo mawili utakayopangiwa.
- Ongoza kipindi cha mahojiano kwa kila wiki, ukiweka mazingira ya uwazi wako mwenyewe.

### Kwa Wanandoa Wanaofanya Kazi ya Kuelekeza

- Wasaidie wanandoa wanaoelekeza kama ulivyoagizwa.
- Kutana nao kila wiki kwa ajili ya maombi na kujisomea.
- Kama hutakubaliana na wanandoa wako wanaoelekeza, tafadhali jadiliana nao kwa siri, siyo mbele ya kikundi.
- Wasaidie wanandoa wanaoelekeza kukamilisha kazi zo zote zilizopo kila baada ya kipindi.
- Hudhurieni mikutano ya uhamasishaji ya ***2=1***.

Huu ni wakati wako wa kujiandaa kuwa Wanandoa Waelekezaji. Angalia, sikiliza, na pata ushauri na masahihisho kwa moyo mweupe. Faidika na wiki zote mnazokutana kwa pamoja. Wakati huu uwe unafikiria jinsi gani Mungu anaweza kuitumia nyumba yako kama kituo cha kuwafikia wengine. Jiandae na kujifunza sasa na uwe tayari kuondoka na kwenda kufundisha kikundi chako cha Ndoa ni ya Kudumu baada ya kozi hii kukamilika.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 9 – NGUVU YA UKARIBU WA KIMWILI

**LENGO:** Kuuelewa umuhimu wa umoja wa kimwili kati ya mume na mke, kupata mwanga wa mtazamo wa Mungu kwa ajili ya tendo la ndoa, na kujifunza jinsi ya kuendeleza na kukuza mahusiano yetu ya kimwili.

**MAELEKEZO:** Uwe wazi kwa Bwana anayetaka kuponya majeraha na maumivu makali katika eneo la tendo la ndoa katika maisha ya wanandoa. Uwe tayari kushirikiana na wanandoa baada ya kipindi kuwasaidia ili wafunguliwe.

**KULENGA KUOMBEA**: Ombea wale walio na majeraha ya nyuma na matatizo ya tendo la ndoa. Omba kwa ajili yao ili waelewe umoja wa kimwili alioukusudia Mungu. Endeleza maombezi yanayoongozwa na Roho. Endelea kuwaombea wanandoa wako kwamba waongozwe na Roho katika utoaji wao. Wasiliana na wanandoa wale ambao wameonesha kuwa tayari kuwa Waelekezaji katika Mafunzo au peleka majina yao kwenye Timu yako ya Viongozi ya Uelekezaji kama wanajali. Ni wakati wa kuanza kuomba kuhusu Uelekezaji.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI ZA KILA WIKI✦

## Siku ya Mahafali

Kabla hujajua darasa hili litahitimu na utakuwa muda wa wanandoa wako kuhitimu. Kwa hiyo, anza kupanga mambo ya tukio la kuhitimu sasa.



Je, kuna mahali ambapo pameandaliwa? Mahafali inaweza kufanyika kwenye jengo lo lote la wazi au kanisani, ila tunashauri achana na vifaa vya kukodi kwa pesa.

Makanisa mengi hutoa majengo yao bila gharama. Pia kuna vituo vya kijamii au klabu ambavyo vinaweza kutolewa bure. Mara nyingi matukio haya huhudhuriwa na watu wengi, hivyo ni vizuri kupanga mapema.



TAFADHALI ZINGATIA: Kama kundi lako litachagua vifaa au jengo la kukodisha, kundi ndilo lilipe gharama hiyo. Isitolewe kwenye matoleo.

Je, vyeti vimewasili? Kagua majina na hakikisha kwamba viko sahihi.

Je, wanandoa wako wako tayari kuwashirikisha wengine habari za maisha yao? Hakikisha wanapewa mwongozo ulionao kwenye kifurushi cha darasa.

Watie moyo kukaribisha famila zao na marafiki zao. Hili ni tukio maalumu sana na wangependa kuwashirikisha wengine. Waruhusu wanandoa wa kikundi chako kukaribisha wanafamila wao na marafiki zao. Kwenye kitabu chao kuna sehemu ya kuorodhesha majina ya wale wanaotaka kuwakaribisha.

Waombe wawakaribishe wachungaji wao pia. Pia unaweza kupata majina kutoka Ofisi ya Kitaifa ya Wanandoa ambao wangependa kusikia habari za huduma hii. Hakikisha wamepewa mwaliko na wachungaji walioko kwenye eneo lako ambao wanavutiwa na huduma hii.

Kadi za ukaribisho na matangazo vinaweza kuagizwa kutoka makao makuu. Matangazo yanaweza kubandikwa kwenye makanisa, sehemu mbalimbali za wazi, n.k, kwenye jumuia yako. Tafadhali agiza vifaa hivi na tafadhali usivirudufishe.

**Wanandoa Waelekezaji**

Mpaka sasa unaweza kuwa umegundua kwamba kuna wanandoa kwenye kikundi chako ambao wanaweza kuwa waelekezaji wazuri tu. Kwa nini usiseme nao? Wanaweza kufundishwa ili wafundishe darasa – Ndoa ni ya Kudumu, ni wazazi daima, au MMOJA daima. Au wanaweza kufundishwa au kupigiwa simu ili kuelekeza wanandoa wanaojisomea wao wenyewe au kujisomea kwa vikundi. Wanaweza kuelekeza wanandoa kwa njia ya baruapepe au simu kwa njia ya sauti au video. Fursa hazina kikomo. Kama wana moyo wa kufanya kazi na wanandoa wengine, tuna njia ya kuwawezesha kufanya hivyo.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 10 – NGUVU YA VITA VYA KIROHO

**LENGO:** Kuwafundisha wanandoa jinsi ya kupigana vita vya kiroho kama mwili mmoja. Kuboresha umakini wa vita endelevu vya kiroho tulivyo navyo, kuwaelewesha wanandoa ili wazijue silaha na matumizi yake, na kujifunza kugundua mashambulizi ya adui yanapotokea.

**MAELEKEZO:** Jiandae dhidi ya adui anapochochea mambo. Analichukia somo hili! Jiandae kiroho kuwahudumia watu wanaohisi "hupaswi kuzungumza kuhusu mwovu."

**KULENGA KUOMBEA:** Mara nyingi hii huwa ni wiki ya vita vikali. Endea kufanya maombezi hasa kadiri Roho Mtakatifu anavyokuongoza. Anza kuombea huduma yako ya kuwafikia wengine. Omba kwamba wanandoa wako wasimame pamoja kwa ajili ya ndoa za wengine kwa kusaidia kifedha wiki hii.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI ZA KILA WIKI✦ Siku ya Mahafali

Darasa lako likikamilisha, lazima ufanye sherehe ya mahafali. Huu ni muda maalumu kwa wanandoa darasani kwako pia kama muda wa taarifa kwa wale wanaovutiwa kujua zaidi kuhusu 2=1 na, hasa kozi za Ndoa ni ya Kudumu.

Hii ni fursa kwa kila mwanandoa kushirikisha kile ambacho Mungu amekifanya katika maisha yao kwa wiki zote zilizotangulia.

Vyeti vya kuhitimu hugawiwa kwa wanandoa wote ambao bado hawajapokea katika kikundi kingine. Unapaswa kuwa na vyeti vyote mpaka sasa. Kama huna vyeti hivyo, tafadhali ijulishe ofisi ya kitaifa. Vyeti havitumwi kama kuna gharama za uandikishaji hazijalipwa katika kikundi hicho, au kama taarifa za kila wiki hazijafika kwenye ofisi ya kitaifa. Kadiri mambo haya yanavyoshughulikiwa, vyeti hutumwa kwako. Umepokea kifurushi cha Mahafali. Ndani ya kifurushi hicho kuna fomu zote na maelezo.

Umepokea Kifurushi cha Mahafali. Katika kifurushi hicho utapata fomu na vifaa vingine vinavyohitajika. Utapata maelekezo katika sehemu hii ya Fomu kwa ajili ya kamilisha kujaza kila fomu na taarifa za jinsi ya kuendesha kikao.
.
Mpangilio wa kikao ni utaratibu unaotolewa kama ushauri tu. Unaweza kuwasilisha maelezo hayo kwa mpangilio wo wote ule ambao utajisikia vizuri kuutumia na kwa kundi lako. Hakikisha unavihusisha vipengele vyote vilivyoorodheshwa. Kikao kisizidi masaa mawili, hivyo ni vuzuri kuandaa maelezo na kujali muhtasari wako uliouandaa. Wanandoa wote wanaotamani kujiunga na na darasa la ***2=1*** wanapaswa kusikia malengo ya huduma na jinsi darasa linavyoongozwa. Njia ya haraka na rahisi ya kutekeleza hili ni kuwaruhusu wahudhurie mahafali ambapo hayo yote hufafanuliwa vizuri. Wanaweza kujisajili kwa ajili ya darasa mwishoni mwa kikao. Kama unahitaji kukutana mwanandoa binafsi ili uweze kujaza darasa, hakikisha kuwa umekamilisha mambo yote ya muhimu. Hairuhusu mwanandoa kuanza darasa la 2=1 bila kuelewa nini watapokea na nini kinahitajika kutoka kwao.

1. UKARIBISHO
2. MAOMBI
3. SIFA NA IBADA
4. MAONO YA ***2=1*** *
5. WANANDOA WANASHIRIKISHA HABARI ZAO
6. ITIFAKI YA DARASA *
7. FURSA YA UTOAJI
8. MASWALI NA MAJIBU *
9. HUDUMA
10. USAJILI

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 11 – NGUVU YA MABADILIKO

**LENGO:** Kuwasaidia wanandoa kuratibu zana zote walizopokea katika Ndoa ni ya Kudumu ili waendelee kukua katika ndoa zao kama Mungu anavyokusudia, kuonesha umuhimu wa kuziachilia dhambi zilizofichika katika ndoa zao, na kuwapa kielelezo ambacho juu yake wanaweza kujenga nyumba zao zenye nguvu.

**MAELEKEZO:** Mwishoni mwa somo hakikisha kwamba unawarudisha wanandoa katika maono ya nyumba zenye nguvu ambayo Mungu anataka. Wakumbushe kukamilisha kile walichokianzisha

**KULENGA KUOMBEA:** Endelea kuandaa usiku wa mahafali. Omba kwa mapenzi kamili ya Mungu kwa kila mwandoa kwa hatua yao inayofuata. Omba kwamba wanandoa wako wanaunda ruwaza mpya za ukarimu katika utoaji wao wa fedha.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦ Mahafali

UKARIBISHO

Hakikisha wageni wamesalimiwa na kujisikia wamekaribishwa.

MAOMBI


Fungua kwa maombi mafupi.

SIFA NA IBADA

Iwe rahisi tu kwa nyimbo chache. Uwe makini na watu waliohudhuria.

MAONO YA ***2=1***

**Mapendekezo ya kuwashirikikisha wengine**: Nyumba imara hufanya jamii iliyo imara. Kwa sasa familia nyingi zinakumbwa na matatizo mengi magumu ambayo mara nyingi huzifanya zisiendelee kukua kuwa nyumba imara. Utume wa ***2=1*** ni kuwasaidia wanandoa kujenga ndoa yenye afya kwa kupitia mafunzo na maelekezo ili kwamba familia zao ziweze kuwa imara. Tunataka kukusaidia wewe uweze kuwa na ndoa yenye afya na imara ili ukamilishe hatima yako.



Kozi za Ndoa ni ya Kudumu siyo jibu la kichawi. Kuhudhuria vipindi inahitaji kwamba wanandoa wawe tayari kufanyia kazi mahusiano yao kila siku. Mara zote siyo rahisi, lakini tunaamini kwamba kweli iliyomo kwenye kozi hii itageuza au itabadilisha ndoa yo yote ile haijalishi ni “nzuri” au “mbaya” kiasi gani kwa kuanzia.

Wanandoa waelekezaji wa ***2=1*** wanahudumia ndoa na familia ulimwenguni kote, katika mataifa zaidi ya 90 na lugha 41.

WANANDOA WASHIRIKISHANE HABARI ZAO

Waruhusu wanandoa wako washirikishane kile kilichotokea katika mahusiano yao kama matokeo ya darasa hili.

ITIFAKI YA DARASA

Eleza jinsi kozi za Ndoa ni ya Kudumu zinavyofanya kazi: urefu wa kozi na maudhui yake, mwanandoa atarajie nini kila wiki, wajibu gani unatakiwa, n.k.

FURSA YA KUTOA

Wape wanandoa fursa ya kutoa mchango kwa ajili ya huduma ya kiulimwengu ya 2=1. Michango yao huwezesha kufikia ndoa na familia zaidi ulimwenguni kote.

MASWALI NA MAJIBU

Wape fursa watu ya kuuliza maswali.

HUDUMA

Pata muda wa kuwahudumia wanandoa wanaohitaji msaada.

# MAMBO YA KULENGA KUOMBEA KWA WIKI

**Wakati Timu ya Waelekezaji Ikikutana Kuomba**

## WIKI YA 12 – NGUVU YA MOJA

**LENGO:** Kuwapa changamoto wanandoa kutoa kile walichokipokea, kuwasaidia kuanza kuwaza kuhusu kazi ya Mungu kwa ajili yao.

**MAELEKEZO:** Wasilisha somo na uwape changamoto ya kwamba Mungu ana mpango kwa ajili yao. Watie moyo hata wanandoa walio na maumivu kumtafuta yeye kwa ajili ya ndoa yao. Watie moyo wanandoa kukamilisha Mkazo Maishani wa wiki hii ifikapo usiku wa mahafali. **Kama unapanga kitu maalumu kwa ajili yao, waambie jinsi ya kujiandaa.**

**KULENGA KUOMBEA:** Omba kwa ajili ya kila mwanandoa aweze kusikia kazi yake kwa uwazi. Funda kila hila na kazi za yule adui ambazo zinaweza kuwazuia wasisikie kutoka kwa Mungu. Ombea wanandoa wapokee kikamilifu kile ambacho Bwana amewaandalia wakati wa kikao cha mwisho cha huduma.

## ✦DOKEZO ZA UELEKEZAJI KWA KILA WIKI✦ Sasa Nini?

Kama ungependa kuwa na jioni maalumu kwa ajili ya kuombea wanandoa wako baada ya kuwa wamekamilisha Mkazo Maishani wa wiki hii, wajulishe sasa. Baadhi ya waelekezaji wa wanandoa huandaa chakula cha jioni, wengine hufanya mambo ya kipekee sana kama vile kutawadha miguu. Waelekezaji wengine wa wanandoa huombea kulingana na kile ambacho Mungu amewafunulia. Wengine huwaruhusu wanandoa kushirikisha kila ambacho Mungu amesema nao wakati wakiomba pamoja kwa ajili ya wito wao wa pamoja. Ni juu yako.

Kadiri unavyokaribia mwisho wa kipindi, utagundua kwamba wanandoa wengi wanataka kuendelea kukutana pamoja. Kuna maoni mengi ya kufikiria.

1. ***Viako vya mara kwa mara na wahusika***
   Endeleeni kukutana pamoja kama kikundi mara kwa mara. Chakula cha jioni ni njia nzuri sana ya kuweza kuwakutanisha tena. Wanandoa wanaweza kutaka kukutana pamoja na watoto wao. Kama ni hivyo, fikiria mpango wa kuwa na pikiniki au kambi au shughuli nyingine ambayo watoto watarufahia pia.
2. ***Kutana pamoja na wahitimu kutoka madarasa mengine***
   Ungependa kukutana na wahitimu wengine katika vikao vinavyohusisha watu wengi kwa ngazi ya mji au jiji. Hii hutoa fursa ya kukutana na wanandoa wengine na kupanua wigo wa mawasiliano.
3. ***Mwe na vikao vya mara kwa mara kwa ngazi ya jimbo au kanda***
   Hii hutoa fursa kwa wanandoa kukutana na wengine kutoka ngazi ya jimbo au kanda au maeneo mengine. Hii inaweza kufanyika kila robo mwaka katika eneo lenu.
4. ***Tumia maelezo mengine ya 2=1 na unda vikundi vya majadiliano***
   Wanandoa wanaweza kununua CD, DVD, na vifaa vingine vya kufundishia kutoka ***2=1*** na kuanzisha vikundi vyao vya majadiliano. Hii ni njia nzuri sana ya kuweza kuwafikia majirani zao na familia zao.
5. ***Wanandoa waliozaliwa mara ya pili wakati wa kipindi na wasio na kanisa, ni vizuri wafikirie kujiunga na kanisa.***
   Hii itawapatia fursa ile ile ya kukutana na watu kama walivyokuwa wamezoea wakati wa vipindi vyetu na wanaweza kuendelea kukutana na wanandoa wengine waliozaliwa mara ya pili wakati wa vipindi vyetu. Kuna makanisa madogo madogo yanayoanzishwa ulimwenguni kote.